Je, unaye rafiki aliye na ualbino?

Je, unaye rafiki anayeonekana kama mzungu kuliko kama wewe? Labda mko katika darasa moja au labda ni mtoto wa jirani? Au labda ni ndugu au dada? Labda ni mtoto katika jamii?

KWANINI MTOTO HUYO NI MWEUPE SANA?

Umewahi kufikiri kwanini mtoto huyo anayo sura tofauti na watoto wengine? Kwanini ngozi na macho yake ni meupe sana? Kwanini nywele yake ni ya manjano sana?

MTOTO HUYO SI MGONJWA. MTOTO HUYO NI BARAKA KAMA WEWE.

Mtoto huyo sio mgonjwa kwa sababu ni mweupe hivyo. Yeye anayo hali inayoitwa ualbino. Ualbino si ugonjwa. Haisababishwi na viini. Hakupata ngozi na macho yake hiyo nyeupe kwa “kuambukizwa,” kama vile watu “wanavyoambukizwa” magonjwa. Hakuna mtu anayeweza “kuambukizwa” ualbino kutoka kwa mtu. Hauwezi kubadilika kuwa mwekundu kwa kuwa karibu na mtoto aliye na ualbino. Hauwezi kubadilika mwekundu kwa kumgusa.

Ualbino haisababishwi na mizungu au miungu. Mtoto aliye na ualbino ni baraka kama wewe ulivyo baraka. Aliumbwa kwa mfano wa mungu kama wewe ulivyo umbwa.

UALBINO NI NINI?

Kwa hivyo ni kwa nini ngozi ya rafiki yako ni nyekundu?

Hii ni kwa sababu ngozi yake haina rangi-rangi inayoitwa melanin. Kwa hivyo ngozi yake haina rangi, na damu yake yaweza kuonekana kidogo kupitia ngozi yake. Hii hufanya ngozi yake kuonekana nyekundu. Hii ni hali inayoitwa ualbino. Ni hali wala sio ugonjwa. Hali humaanisha “hivi ndivyo watu huwa.” Ni hali

inayoitwa ualbino, ngozi haiwezi kutengeneza rangi, kwa hivyo mtu huonekana mweupe au mwekundu.

AINA MBALIMBALI NI NJEMA. MUNGU ANAIPENDA.

Mungu anapenda aina. Yeye aliwaumba watu wa aina na rangi mbalimbali duniani na Yeye anawapenda wote. Mungu alimuumba rafiki wako albino naye anampenda mtoto huyo kama anavyokupenda. Si basi haitakuwa hali ya kuvutia, au dunia isiyopendeza, ikiwa maua yote yangekuwa na rangi moja? Au kama vipepeo wote wangefanana? Au kama watoto wote wangefanana? Mungu anapenda sura za rangi zote. Aliziumba rangi zote nazo zampendeza. Watoto walio na sura nyeusi kama makaa ni sura nzuri kwake, pia wale walio na rangi ya maji ya kunde au wale ambao ni weupe au wekundu kama maua. Aliziumba rangi hizi zote. Alimuumba rafiki wako albino vile alivyo, naye anampenda vile alivyo.

WATU WENGINE HAWAELEWI

Ikiwa wengine wanaonekana kumwogopa rafiki yako wakati mwingine, ni kwa sababu hawaelewi ualbino ni nini. Watu mara nyingi huogopa wasioelewa. Rafiki yako albino anaonekana tofauti na wengine, lakini ni kama wewe kwa njia nyingi.

RAFIKI YAKO AWEZA KUFANYA KAZI ZA MANUFAA KWA MAISHA YAKE KAMA WEWE

Watu wengi walio na ualbino wamekuwa watu waliofanya mambo makuu. Wengine ni wanamuziki wanaojulikana, watu wa serikali na wanabiashara wengine pia ni waalbino. Na kwa msaada wake Mungu, rafiki yako albino anaweza kufanya chochote ambacho watu wengine wanachoweza kufanya. Urafiki wako na kumpa moyo utasaidia pia.

Watu wengi wenye ualbino wanayo akili nyingi. Wanaweza kujifunza kama wengine. Wanaweza kwenda shuleni. Wanaweza kufanya vyema katika masomo yao.

Every Child Ministries

Prepared by Every Child Ministries
Ukurasa umetayarishwa na Huduma ya Kila Mtoto
"Kwa watoto wa Afrika Waliosahaulika"
Barua Pepe : ecmafrica@ecmafrica.org
Maelezo ya Kiswahili na: Lindah Kotut

RAFIKI YAKO ANAWEZA KUISHI MAISHA MAREFU

Watu walio na ualbino wanaweza kuishi hadi uzeeni kama watu wengine. Kumbuka, ualbino sio ugonjwa.

NINI RAFIKI YAKO ANAWEZA KUFANYA KUHUSU CHANGAMOTO ANAZOKUMBANA NAZO

Kuna shida mbili ambayo watu wenye ualbino hukumbana nazo, pia kuna vitu wanavyoweza kufanya ili kuimarisha shida hizi. Waweza kumsaidia rafiki yako kwa kumpa moyo kufanya mambo yanayoweza kumsaidia.

KWANZA – RAFIKI YAKO AYAYO MACHO NYETI

Kwanza, rafiki yako albino anayo macho ambayo huathirika kwa urahisi kwa mwanga na waweza kuchomeka kwa urahisi. Yeye hana melanin inayokinga macho ya wengine kutokana na madhara ya jua. Yeye anaweza kukinga macho yake kwa daima kuvaa miwani ya giza anapotoka nje wakati wa mchana. Kama rafiki, unaweza kumsaidia kwa kuelewa kwamba rafiki yako anahitaji miwani hii. Ikiwa atakosa kuivaa, macho yake yatachomeka na kuona kwake kutaharibika zaidi. Kama rafiki, usiwatusi wala kuwachokoza watoto waalbino kwasababu wamevaa miwani hizi za giza. Usiwaite “macho nne” au majina mengine. Tafadhali wakumbushe kuvaa miwani zao.

Rafiki yako aweza pia kuvaa kofia iliyo na upana mkubwa ambayo yaweza kukinga macho yake. Wakristo wanaompenda Yesu wametuma zawadi za miwani za giza kwenda kwa kila mtoto aliye na ualbino. Rafiki yako anaweza kupata miwani hizi kwa kuwasiliana na Huduma ya Kila Mtoto. Tunatumaini miwani hizi zitasaidia macho yao.

Maono ya rafiki yako yanaweza kuwa mabaya kwa njia nyingine pia. Ikiwa anayo shida ya kuona shuleni, mpe moyo rafiki yako ili kumwuliza mwalimu ikiwa

anaweza kumruhusu asonge karibu na mbele ya darasa. Anaweza kuona vizuri kiasi ikiwa ataketi karibu na ubao.

PILI – RAFIKI YAKO ANA NGOZI NYETI

Pili, rafiki yako anayo ngozi nyeti inayoweza kuchomeka kwa urahisi. Hii ni kwa sababu rangi ya ngozi yetu inasaidia kwa kutukinga kutokana na madhara ya jua, lakini rafiki yako hana rangi ya ngozi au kinga kwa ngozi yake. Kwa sababu hizi, ngozi yake na mdomo yaweza kupata vidonda kwa urahisi sana ikiwa hatakinga ngozi yake kutokana na jua. Ingawa ualbino sio ugonjwa, waalbino wengi hupata vidonda kwa sababu ngozi zao hazina kinga kutokana na madhara ya jua.

Waweza kufanya mambo kadhaa kumsaidia rafiki yako kutokana na jua. Kwanza, rafiki yako anatakiwa kujizuia kwa jua kutoka saa nne asubuhi hadi karibu saa tisa mchana. Kati ya saa hizi, kupita saa za mchana, mianga ya jua huwa ni joto zaidi na yaweza kumwathiri zaidi. Katika wakati huu, waweza kumpa moyo rafiki yako kubaki ndani ya nyumba au kwenye kivuli kama iwezekanavyo.

Rafiki yako anaweza pia kuvaa nguo zenye mikono mirefu. Shati zenye rangi nyeupe na surali ndefu zitakinga ngozi yake na kurudisha mianga ya jua. Anatakiwa kufunga vifungo vyote. Anaweza kuvaa kofia pana ili kukinga uso na masikio yake. Anaweza pia kujipaka mafuta ya kujikinga kwa jua. Ni muhimu sana kufanya hivi kwa ngozi isiyofunikwa. Waweza kusaidia kwa kutomtusi rafiki yako kwa ajili ya kuvaa nguo zinazofunika kuliko kawaida. Unaweza pia kuwazuia watoto wengine wasimchokoze pia. Unaweza kumkumbusha rafiki yako kuvaa nguo anazohitaji ili kujikinga. Anaweza kuhisi vibaya kwa sababu anatakiwa kuvaa mavazi tofauti na watoto wengine. Unaweza kumpa moyo ya kwamba hii ni muhimu kufanya.

MUNGU ANAMPENDA RAFIKI YAKO ALBINO

Mungu anampenda rafiki yako albino kama anavyokupenda. Rafiki yako ni muhimu kwake, na wewe ni muhimu kwake pia. Anampenda rafiki yako jinsi alivyo, na pia anakupenda wewe jinsi ulivyo. Rafiki yako anaweza kuwa baraka kwa familia yake na dunia kwa ujumla. Wewe waweza kuwa baraka pia.

JE UNAYO MASWALI?

Ni maswali gani unayo kuhusu tuliyozungumza, au kuhusu rafiki zako waalbino? Unaweza kutuma maswali yako kwa Huduma ya Kila Mtoto kwa anwani ya barua pepe tuliyowapa hapa chini. Tutafanya kila juhudi kujibu maswali yako.

Ni shida gani zinazowakumba rafiki zako waalbino? Sisi katika Huduma ya Kila Mtoto tatapenda kuyasikia hayo pia. Tunataka kuona kama tunaweza kusaidia kwa njia yoyote. Wewe na rafiki zako waalbino mwakaribishwa kutuandikia.

AHSANTE

Ahsante kwa kuwa rafiki wa watoto waalbino katika familia yako, katika shule yako, na katika jamii yako. Wakati mwingine watu wasioelewa kuhusu ualbino ni wabaya sana kwa watoto hawa. Watoto hawa wanahitaji marafiki. Wanahitaji upendo na uhusuano. Wewe waweza kuwa baraka kubwa kwa kuwa rafiki yao. Kwa vile tunasema AHSANTE SANA kwa ajili yako!

Mungu akubariki,

Kutoka kwa rafiki zako kutoka “Huduma kwa Kila Mtoto”
Huduma ya Kikristo isiyo ya kiserikali inayoleta tumaini “Kwa watoto wa Afrika waliosahaulika”
Kwa sababu watoto ni rasilimali kubwa zaidi ya nchi yoyote –
Hazina ya thamani kutoka kwa Mungu!

PO Box 28080

Every Child Ministries

Prepared by Every Child Ministries
Ukurasa umetayarishwa na Huduma ya Kila Mtoto
"Kwa watoto wa Afrika Waliosahaulika"
Barua Pepe : ecmafrica@ecmafrica.org
Maelezo ya Kiswahili na: Lindah Kotut

Kampala, Uganda

Barua Pepe: ecmuganda@yahoo.com

Ikiwa upo katika darasa la tano kwenda juu, na ikiwa ungependa kupata maelezo ya undani zaidi kuhusu rafiki yako aliye na ualbino, waweza kuandika barua kwa Huduma ya Kila Mtoto na uwaulize maelezo zaidi. Mungu akubariki!